“Nita” Za Kristo

na

Ellis P. Forsman

“Nita” Za Kristo

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

“Nita” Za Kristo

Yohana 6:31-40

Tunapenda neno la mtu liwe kifungo chake.

Yesu alikuwa mkuu katika hili. Alitoa ahadi nyingi na kuyatimiza yote.

Kwa wakati huu tunataka kuangalia sehemu sita ambapo aliahidi, “*Nita*”.

Tunaweza kuweka imani zetu katika ahadi hizi.

“Sitamtupa nje”

Yohana 6:37, “*Wote anipao Baba watakuja kwangu wala ye yote ajaye kwangu sitamtumpa nje kamwe.*”

Yesu aliahidi wokovu kwa wale watakaomjia kwa maneno yake.

Uwezo huo alipewa na Baba yake wa mbinguni.

- Math. 17:1-5, “*Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani; akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang’aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Na tazama wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye. Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye, msikieni yeye.*”
- Math. 28:18, “*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*”
- Waeb. 5:9, “*Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*”

Ni <u>waumini waliowaaminifu</u> (wafuasi) ambao <u>Yesu aliahidi kuwa hatawatupa nje</u> ya mji pamoja naye mbinguni.

“Nitalijenga kanisa langu”

Math. 16:13-19, “*Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria Filipi akawauliza wanafunzi wake akasema,watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani? Wakasema wengine hunena u Yohana mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmoja wapo wa manabii. Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simon Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simon Baryona kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*”

Tunapata katika Matendo 1-2 kwamba Yesu alitimiza ahadi hii. Petro alipotoa hotuba ya kwanza baada ya Kristo kuanzisha kanisa lake, ambapo nafsi 3000 zilizidishwa.

Yesu alihaidi kwamba milango ya kuzimu haitalishinda. Washiriki mmoja baada ya mwingine watakuja na kwenda, lakini kanisa mara zote litakuwepo; hatakama kuta kuwa na waliobaki atakapokuja kwa mara ya pili.

“Nitamtuma Roho Mtakatifu.”

- Yohana 16:7, “*Lajini mimi nawaambia iliyo kweli yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu.*”
- Yohana 16:13, “*Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*”

Pia tunaona kwa kusoma katika Matendo sura ya 1 na ya 2 kwamba Yesu alitimiza ahadi hii ya kumtuma Roho Mtakatifu ili awaongoze Mitume katika kweli yote.

Sisi hatuongozwi ili kuongeza ukweli wowote katika neno la Mungu, kwa sababu kazi hiyo tayari imesha timizwa.

- 1 Yohana 2:24, “*Ninyi basi, hilo mlilolisikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu, ninyi nanyi mtakaa ndani ya Mwana, na ndani ya Baba.*”

- 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"
- 1 Wathes. 5:21, "*Jaribuni mambo yote; lishikeni lililojema.*"
- Ufu. 22:18-19, "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji takati ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Ahadi ya Yesu kumtuma Roho Mtakatifu kuongoza neno tayari imeshatimizwa.

"Nitawavuta kwangu"

Yohana 12:32, "*Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.*"

Huu ni uwezo wa kisumaku wa Yesu.

- Yohana 6:44-45, "*Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; name nitamfufua siku ya mwisho. Imeandikwa katika manabii, Na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba huja kwangu.*"
- 1 Wakor. 1:18, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu.*"

Kwa sababu Yesu alizichukua dhambi zangu msalabani na kuahidi mji wa milele kwa waaminifu, hakika ninashukuru sana na ninavutwa kusikiliza maagizo yake jinsi ambavyo nitaweza kufika huko.

"Nitawapokea kwangu"

Yohana 14:1-4, "*Msifadhaike mioyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mnamakao mengi kama sivyo ningaliwaambia maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia.*"

Yesu tayari alishawaambia wanafunzi wake kuwa alikaribia kutoa uhai wake kwa wale wanao mfuata. Hivyo, wote walishitushwa na ujuzi huu. Alafu anawatia nguvu kwa kuwaambia kuwa makazi yanawasubiri mbinguni kama watamwamini.

Wengi wa Wakristo wa kwanza walitakiwa kuvumilia mambo magumu (kuubeba msalaba wa Yesu) katika imani yao kwa Bwana wao na Mwokozi. Walikuwa tayari kufanya hili kwa sababu ya ahadi ambayo Yesu aliwaahaidi.

Ahadi hii bado itatimizwa.

"Nitawapa pumziko"

- Math. 11:28, "*Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*"
- Tito 3:7, "*Ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.*"
- 1 Petr. 1:4-5, "*Tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.*"
- 1 Petr. 1:9, "*Katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani wokovu wa roho zenu.*"
- 1 Yohana 2:25, "*Na hii ndiyo ahadi aliyotuahidia, yaani, uzima wa milele.*"

Hitimisho

Kumbuka, Kristo amefanya mengi sana.

Ameweka ahadi nyingi. Baadhi tayari ameshatimiza.

Ahadi zingine bado yatatimizwa, lakini uwe na uhakika zitatimizwa.